# *BARUA #11; USIFIKIRI KWA UHABA, FIKIRI KWA UTELE.*

Karibu rafiki yangu mpendwa kwenye barua yetu nyingine kwenye mfululizo wa barua za mafanikio.

Hizi ni barua za kutupa mabadiliko makubwa ya kifikra na kutupa hatua tofauti za kuchukua ili kuweza kuyafikia mafanikio makubwa tunayoyataka.

Kwenye barua hii tunakwenda kujifunza kuhusu kufikiri kwa utele badala ya kufikiri kwa uhaba.

Tumekuwa tunajifunza na tunajua jinsi fikra zetu zilivyo na nguvu kubwa, tunakuwa kile tunachofikiri na tunapata kile tunachofikiri kwa muda mrefu.

Kama mtu unafikiri kwa uhaba, kwenye kila kitu utaona uhaba, na kama utafikiri kwa utele, kila mahali utaona utele.

Kwa kubadili tu fikra zako kutoka kwenye uhaba na kwenda kwenye utele, unakuwa umeondoka kikwazo kikubwa kwa mafanikio yako.

Karibu kwenye barua, ujifunze, ubadili fikra zako na uanze kuchukua hatua za tofauti.

**Kwenye barua hii tutajifunza yafuatayo;**

KWA NINI TUNAFIKIRI KWA UHABA.

MADHARA YA KUFIKIRI KWA UHABA.

- Utumwa.
- Vita.
- Mfumuko wa bei na anguko la uchumi.
- Ushindani.

ASILI HAINA UHABA.

SAYANSI IMELETA MAPINDUZI YA KWELI.

USHISINDANE, BALI TAWALA.

JITAMBUE NA TENGENEZA UKIRITIMBA WAKO.

FUNGUA FIKRA ZAKO KWENYE UTELE.

HITIMISHO.

# KWA NINI TUNAFIKIRI KWA UHABA.

Kufikiri kwa uhaba ni kama tabia ambayo tunazaliwa nayo, iko ndani ya asili yetu na ndiyo maana ni kitu ambacho tumekizoea na ni kigumu sana kuvunja.

Ukitaka kujua hili liko ndani yetu, pita kwenye duka na ukute kuna kitu kizuri kinauzwa na ukaambiwa kimebaki kimoja tu, mara moja unapata msukumo wa kutaka kukinunua, hata kama ulikuwa hujapanga kununua kitu hicho. Kinachokusukuma kununua ni ile hali ya uhaba ambayo iko ndani yako, kwa kuwa umeambiwa kimebaki kimoja, unaona usipochukua hatua sasa utakikosa na hivyo kutokukipata tena.

Kufikiri kwa uhaba kumejengeka ndani yetu kupitia mageuzi (evolution). Watangulizi wetu waliishi kwenye dunia yenye rasilimali zenye ukomo, hivyo vitu vilikuwa na uhaba mkubwa.

Charles Darwin kwenye nadharia yake ya mageuzi kwa uchaguzi wa asili (Natural Selection) anaeleza hili vizuri. Kwamba kwa kila jamii, viumbe wanaozaliwa ni wengi kuliko

rasilimali zilizopo. Hivyo wote wanaozaliwa hawawezi kupata rasilimali muhimu wanazohitaji, hivyo kunatokea ushindani na wale wenye nguvu zaidi ndiyo wanaoshinda (survival of the fittest), wasio na nguvu wanashindwa na kufa.

Hivyo watangulizi waliopona na wakapitisha sifa hii kuja kwetu ni wale ambao walikuwa wanauona uhaba haraka, wanatumia nguvu zao kuhakikisha wanapata wanachohitaji na wakaweza kupona.

Hivyo tumerithi sifa ya kuona uhaba na kupambana ili tusikose yasiyo muhimu.

Na uhaba ulikuwepo kweli, chukua mfano wa watu walioishi kwenye kijiji kimoja miaka elfu moja iliyopita, hawakuwa na uwezo wa kwenda mbali kutafuta rasilimali zaidi. Hivyo kitu kama ardhi ilikuwa ni rasilimali yenye ukomo, wachache waliishikilia na wengi wakaishia kuwategemea hao wachache kwenye rasilimali hiyo muhimu.

Kadhalika kwenye chakula, miaka mingi iliyopita hakukuwa na chakula cha kumtosha kila mtu, hivyo wachache wenye nguvu walipoona uhaba, walihakikisha wanapata chakula cha kuwatosha.

Hiyo ilikwenda hata kwenye kuzaliana, hakukuwa na watu wa kutosha wenye sifa zilizohitajika ili kuwa mke au mume bora, hivyo uhaba ulipelekea wachache kutumia nguvu zao kupata wake au waume bora wa kuzaa nao watoto.

Kwa miaka mingi, dunia imekuwa inaendeshwa kwa msingi wa uhaba, hivyo uhaba umekuwa ni tabia ya asili kwetu na iliyo ngumu mno kuvunja.

Popote unapokwenda, ni rahisi kuona uhaba kuliko utele. Hata kama hakuna uhaba, bado akili yako itakimbilia kupima uhaba kuliko utele.

Chukua mfano wa kupanda daladala, hata kama daladala ina nafasi za kukaa 20 na wanaotaka kupanda ni 10, kila mtu atataka awahi kupanda

na hapo watu wataanza kugombania. Yote hiyo ni kwa sababu ya kufikiri kwa uhaba.

Hata kwenye sherehe, pale chakula kinapoandaliwa na watu kupanga mstari kwenda kupata chakula, kila aliye nyuma huchungulia mbele kuona kama vyakula vizuri anavyotaka bado vipo. Hata kama watu watahakikishiwa chakula kipo cha kutosha, bado hawataondoa wasiwasi walionao mpaka wapate chakula.

Mifano ni mingi na wewe mwenyewe umeshaendelea kuona jinsi gani umekuwa unafikiri kwa uhaba kwenye mambo mbalimbali. Siyo kosa lako, ni kama ilivyo kuzaliwa mwanamke au mwanaume, siyo kosa lako, umerithi sifa hizo.

Kadhalika kwenye uhaba, ni tabia uliyoirithi, tabia iliyokuwa na manufaa miaka mingi iliyopita, lakini kwa sasa haina tena manufaa na ni kikwazo kikubwa kwenye mafanikio yako.

# MADHARA YA KUFIKIRI KWA UHABA.

Kama tulivyoona, kipindi cha nyuma, kufikiri kwa uhaba kulikuwa na manufaa, kwani rasilimali muhimu zilikuwa chache na ushindani ukawa mkubwa. Ambao hawakufikiri kwa uhaba walikosa rasilimali muhimu na hilo kupelekea wao kufa.

Lakini kadiri dunia imekwenda, maendeleo mbalimbali yamekuwa yanapatikana na ule uhaba wa rasilimali siyo mkubwa tena kama awali. Lakini kwa kuwa ni mazoea, bado wengi wanaendelea kufikiri kwa uhaba, kitu kinacholeta madhara mbalimbali kwa wengi.

Yafuatayo ni baadhi ya madhara ambayo yamekuwa yanatokana na kufikiri kwa uhaba.

## Utumwa.

Utumwa ni biashara ambayo ilipata nguvu kubwa miaka ya nyuma na hii ilitokana na watu kufikiri kwa uhaba.

Wachache wenye nguvu walijimilikisha njia zote muhimu za uzalishaji kama mashamba

makubwa huku wakiwaacha wengi wakiwa hawana njia za kuzalisha.

Kwa kuwa watu hawakuweza kwenda mbali kutafuta rasilimali hizo, hawakuwa na namna bali kuwa tayari kutumikishwa na wale waliojimilikisha rasilimali hizo.

Hivyo wachache waliotumia nguvu zao kujimilikisha njia za uzalishaji, waliwatumikisha wengi ambao hawakuwa na njia hizo za uzalishaji.

Watu waliteswa na hata kufa katika hali hiyo ya utumwa, kwa sababu tu waliaminishwa kuna uhaba na hawawezi kuishi bila kuwa kwenye hali hiyo ya utumwa.

## Vita.

Vita zote kubwa za dunia na hata vita baina ya mataifa au vita za ndani ya mataifa, msingi wake mkuu uko kwenye uhaba. Lazima kunakuwa na rasilimali muhimu ambayo inaonekana kuwa na uhaba na hivyo kila mtu anaitaka lakini hakuna maelewano.

Tumeona kwenye vita za dunia, kugombea makoloni ilikuwa ni moja ya sababu za vita hizo kuanza na hata kuendelea.

Tunaona pia kwenye nchi zenye rasilimali kubwa kama madini na mafuta, vita za wenyewe kwa wenyewe huwa haziishi kwa sababu rasilimali hizo zinaonekana kuwa na uhaba na kuna kikundi kinaonekana kunufaika kuliko wengine.

## Mfumuko wa bei na anguko la uchumi.

Mifumuko ya bei na maanguko ya kiuchumi huwa yanachochewa na kufikiri kwa uhaba. Pale watu wengi wanapoona kitu kina uhaba, huwa wanataka kuwa nacho kwa wingi zaidi na hilo hupelekea bei ya kitu hicho kupanda. Kutegemea na umuhimu wa kitu, watu wanaweza kuwa tayari kulipia bei ya juu zaidi, kitu kinachopelekea bei ya kitu hicho kuendelea kupanda zaidi na zaidi.

Hilo hupelekea mfumuko wa bei kuwa mkubwa na uchumi kuathirika kwa kiwango kikubwa. Kwa kujua hali hii ya kufikiri kwa uhaba, baadhi

ya wafanyabiashara wanaweza kuchagua kuficha aina fulani ya bidhaa ili kupelekea bei yake ipande zaidi sokoni na wapate faida kubwa.

Maanguko ya uchumi pia yamekuwa yanachangiwa sana na kufikiri kwa uhaba. Kila anguko la uchumi huanza na kukua sana kwa soko la hisa, kitu ambacho hakiendani na uhalisia wa ukuaji wa uchumi. Mfano hisa za kampuni fulani zinaanza kupanda bei, kwa watu kuona ni fursa, kila mtu anakimbilia kuzinunua, kitu kinachofanya bei za hisa hizo kuzidi kupanda bei huku uzalishaji halisi ukiwa haupo.

Kadiri hisa zinavyopanda bei, ndivyo wengi zaidi wanavyokimbilia kuzinunua na ndivyo bei inazidi kupanda. Inafika hatua ambayo bei inakuwa juu sana, wengi wamewekeza na haiwezi kuongezeka zaidi. Hali inapotokea hivyo kwa hisa nyingi, kinachofuatia ni anguko la uchumi mzima.

Kufikiri kwa uhaba kunawafanya watu kuwa tayari kulipa gharama kubwa kitu kinacholeta madhara makubwa kiuchumi.

## Ushindani.

Kufikiri kwa uhaba kimekuwa ndiyo chanzo kikubwa cha ushindani kwenye kila eneo la maisha. Pale watu wanapoona kitu kina uhaba, huwa kwenye hali ya ushindani ili kupata zaidi ya wengine.

Ushindani unapokuwa kwenye mambo ya burudani kama michezo ambapo wachezaji wengi wanashindania nafasi ya juu, huwa ni kitu cha kufurahia.

Lakini ushindani unapokuwa kwenye shughuli za uzalishaji, kama kazi au biashara, huwa hauna manufaa, kwa sababu watu hujikuta wanahangaika eneo dogo na kuacha eneo kubwa lenye thamani kubwa.

Kufikiri kwa uhaba kunatuingiza kwenye ushindani ambao hauna manufaa yoyote kwetu zaidi ya kutuchosha na kutuumiza.

# ASILI HAINA UHABA.

Kutokana na mienendo ya kihistoria, watu mbalimbali wamekuwa wakitabiri kwamba rasilimali muhimu zilizopo zitaisha na hapo maisha hayatawezekana tena duniani. Lakini mara zote mambo yamekuwa tofauti, asili imekuwa haina uhaba bali utele, rasilimali muhimu na tunazohitaji sana hazijawahi kuisha kabisa.

Asili imekuwa inazalisha kadiri watu walivyo na uhitaji. Chukua mfano mdogo wa viumbe tunaowatumia kama chakula kila siku. Chukua mfano wa samaki, kila siku watu wanakula samaki, lakini samaki hawajaisha duniani. Wanaendelea kuzaliwa kwa wingi zaidi.

Hivyo asili haina uhaba, bali ina utele, inaendelea kuzalisha kadiri ya mahitaji ambayo watu wanayo. Na hata rasilimali muhimu zinapoonekana kuisha, asili inatupa mbadala wa rasilimali hizo.

Pamoja na hali hii ya asili kutokuwa na uhaba, bado watu wamekuwa hawaachi wasiwasi

unaotokana na uhaba, kwa kuona kwamba rasilimali muhimu zitakwisha na huo utakuwa ndiyo mwisho wa maisha duniani.

Baadhi ya wanasayansi na wachumi waliona kwa jinsi ongezeko la watu linavyoendelea duniani, itafika mahali dunia itakuwa imejaa kabisa na hakuna tena mahali pa watu kukaa. Lakini mpaka sasa siyo tu kwamba dunia haijajaa, bali pia watu wanaendelea kutafuta makazi nje ya dunia, tafiti mbalimbali zinafanywa kwenye sayari ya Mars kuona uwezekano wa kuwepo kwa makazi ya binadamu huko.

Kwa kipindi kirefu nishati ilionekana kuwa changamoto, pale dunia ilipotegemea sana nishati ya mafuta katika kuendesha shughuli zote za uzalishaji pamoja na nishati nyingine kama umeme. Ilionekana baada ya miaka kadhaa mafuta yanayochimbwa yatakuwa yameisha na hivyo dunia itakosa chanzo cha nishati. Lakini sasa kuna vyanzo mbadala vya nishati kiasi kwamba hakuna uwezekano wa nishati kukosekana kabisa.

Kwa kuanza na nishati ya jua, sasa inaweza kugeuzwa na kutumika kwa njia mbalimbali. Bado kuna nishati ya nyuklia, madini yenye uwezo wa kuzalisha nishati kubwa kwa kutumia kiwango kidogo.

Yote hii ni kuonesha jinsi ambavyo asili haina uhaba, kwa rasilimali zote muhimu inaendelea kuzalisha na kama kuzalishwa zaidi hakuwezekani basi inatupa mbadala wake.

Japokuwa tunaitumia asili kuona uhaba, asili inatudhihirishia kila wakati kwamba haina uhaba, ina utele wa kila rasilimali kadiri tunavyozihitaji.

## SAYANSI IMELETA MAPINDUZI YA KWELI.

Tabiri mbalimbali za uhaba wa rasilimali kuleta anguko kubwa kwenye dunia zimekuwa zinashindwa kwa sababu kuna kitu kimoja ambacho watu hawawezi kukitabiri, sayansi.

Tuchukue mfumo wa ukomunisti uliopendekezwa na kuhubiriwa sana na Karl

Marx, huyu alikuwa mpingaji mkubwa wa mfumo wa ubepari na kuamini kadiri mfumo huo unavyokua, utajiangusha wenyewe na hilo litapelekea kuzaliwa kwa mfumo mpya wa ukomunisti wenye manufaa kwa wote.

Aliandika hayo kwa kutumia mifano ya mfumo wa ubepari wa karne ya 19 ambao ulikuwa ni ubepari wa jadi, ubepari ambao wachache walinufaika kweli huku wengi wakiumia.

Kwenye ubepari huo wa zamani, wamiliki wa viwanda ndiyo walikuwa wamiliki wa njia kuu za uzalishaji na wale ambao hawakuwa na viwanda walikuwa ndiyo wafanyakazi. Mazingira ya kazi hayakuwa mazuri, watu walifanya kazi kwa masaa mengi na malipo yalikuwa madogo.

Maisha ya wafanyakazi yalikuwa magumu huku mabepari wachache wakipata faida kubwa. Marx aliona hilo ndiyo litaua ubepari, maana tabaka la chini litazidi kuwa kubwa huku maisha yao yakiwa magumu, watashindwa kuvumilia

na hivyo kuleta mapinduzi ambayo yataondoa kabisa mfumo wa ubepari.

Ambacho Marx hakuona ni maendeleo ya sayansi na teknolojia ambayo yameboresha sana ufanyaji wa kazi, mazingira ya kazi kuwa salama na hata muda wa kazi kupungua huku malipo yakiongezeka. Japo bado mabepari wanaomiliki njia za uzalishaji wanapata faida kubwa, hali ya wafanyakazi siyo mbaya kama ilivyokuwa awali.

Kingine ambacho Marx na wafuasi wake hawakuona ni uchumi shirikishi kupitia masoko ya hisa. Kwa makampuni kuuza hisa zake kwenye soko, kunafanya hata watu wa chini wawe sehemu ya umiliki na kunufaika na faida inayopatikana.

Chukua mfano mtu ni mfanyakazi wa kiwanda cha magari, ambaye analipwa mshahara mdogo, lakini pia mtu huyo anachagua kununua hisa za kampuni hiyo. Pale kampuni inapopata faida, na yeye anaipata pia. Hali hii imefanya uhasama baina ya tabaka la chini na juu usiwe

mkubwa, kwa kuwa uchumi unawashirikisha wote.

Hivyo fikra zote za uhaba tulizonazo, sayansi imeleta mapinduzi ya kuzivunja na kuziondoa kabisa. Kila eneo la maisha limeguswa na maendeleo ya sayansi. Chukua mfano wa usafirishaji, kipindi cha nyuma watu walikaa eneo moja na kugombea rasilimali chache zilizokuwepo hapo. Lakini baada ya njia za usafirishaji kuwa bora, watu waliweza kwenda mbali zaidi na kukuta rasilimali nyingi ambazo hazina ushindani.

Ugunduzi wa kompyuta, mtandao wa intaneti na simu janja yamekuwa ni mapinduzi makubwa ambayo yamezidi kuondoa ile hali ya uhaba.

Chukua mfano wa biashara, kipindi cha nyuma ilimtaka mtu awe na mtaji mkubwa ndiyo aingie kwenye biashara, lakini kwenye zama hizi za mtandao, kila mtu anaweza kuingia kwenye biashara hata kama hana mtaji kabisa.

Kadhalika kwenye sanaa mbalimbali, kipindi cha nyuma ilibidi mtu akubalike na watu fulani ndiyo aweze kutoa kazi yake ya sanaa, iwe ni kitabu au muziki, lakini kwenye zama hizi za mtandao, kila mtu anaweza kutoa kitabu au muziki wake bila ya kuomba ruhusa kwa yeyote.

Ukija kwenye sekta ya afya, sayansi imefanya mapinduzi makubwa mno, magonjwa mengi yamepata tiba au kinga, umri wa watu kuishi umeongezeka na hata ubora wa maisha umekuwa wa hali ya juu kutokana na ugunduzi mwingi uliofanika kwenye eneo la afya. Magonjwa ambayo kipindi cha nyuma yalikuwa ni tiketi ya kifo kwa wengi, sasa yanatibika au kuzuilika.

Sayansi imeleta na inaendelea kuleta mapinduzi ya kweli, kwa kila uhaba tunaokutana nao, sayansi inatengeneza utele zaidi. Lakini kwa kuwa tunaishi kwenye mazoea, bado tunazidi kuona uhaba.

# USHISINDANE, BALI TAWALA.

Madhara makubwa ya fikra za uhaba kwenye maisha yetu ya mafanikio ni kutupeleka kwenye ushindani. Na ukishaigia tu kwenye ushindani, huwezi kufanikiwa, kwa sababu unatumia nguvu nyingi kuwashusha wengine kuliko kupanda mwenyewe.

Kufikiri kwa uhaba kunakufanya uone rasilimali muhimu unazohitaji hazipo za kutosha hivyo wengine wakizichukua huwezi kuzipata tena.

Kwenye kazi, unaona nafasi za juu ni chache na wanaoziangalia ni nyingi, hivyo ili uipate nafasi hiyo lazima mwingine aikose. Hapo unahakikisha unawazuia wengine wasiweze kupata nafasi hiyo ili iwe yako.

Kwenye biashara unaona wateja ni wa uhaba hivyo usipowazuia wengine kuwapata hutaweza kuwapata.

Katika hali hii ya ushindani, mtu unatumia rasilimali nyingi kuwashusha wengine kuliko unavyotumia kuhakikisha unapanda zaidi.

Matokeo ya ushindani huwa ni watu wote kuishia kwenye eneo moja na hakuna anayeenda mbali zaidi.

Ili kufanikiwa kweli, hupaswi kushindana kwa namna yoyote ile, badala yake unapaswa kutawala. Unapaswa kuchagua eneo ambalo lina utele wa rasilimali muhimu kwako na kisha kulitawala kwa namna ambayo ujio wa wengine hauwezi kukusumbua kabisa.

Unapotawala, huhangaiki na wengine na kutaka kuwashusha, bali unahangaika na wewe mwenyewe na kukazana kupanda juu zaidi.

Unapokuwa na uhakika kwamba kuna utele wa rasilimali muhimu, huwaangalii wengine kama hatari kwako, bali unawaacha wafanye yao na wewe unafanya yako. Nguvu zako unazitumia kwa usahihi kuhakikisha unapata kile unachotaka na siyo kuzipoteza kuhangaika kuwashusha wengine.

Ili uweze kuacha kushindana na uweze kutawala, lazima ujitambue wewe mwenyewe na kisha kutengeneza ukiritimba wako.

# JITAMBUE NA TENGENEZA UKIRITIMBA WAKO.

Hatua muhimu kwenye kuacha kushindana na kutawala ni kujitambua wewe mwenyewe na kutengeneza ukiritimba (monopoly) wako.

Tangu enzi na enzi, wale waliofanikiwa sana walitengeneza ukiritimba kwenye aina ya biashara walizofanya. Japo wengi walifanya hivyo kwa kuwawekea wengine uhaba, wao hawakuona uhaba, waliona utele na kuutawala.

Ukianza na Andrew Carnegie aliyetawala uzalishaji wa chuma, alijenga ukiritimba mkubwa kwenye hilo na hakuna mwingine aliyeweza kuingia.

Ukija kwa John Rockerfeller, alitengeneza ukiritimba mkubwa kwenye biashara ya mafuta kiasi kwamba alimiliki kila kitu kwenye mlolongo mzima wa biashara hiyo.

Bill Gates pia alijijengea ukiritimba kwenye biashara ya programu za kompyuta, huku Steve

Jobs akijijengea ukiritimba kwenye simu za Iphone.

Na kwa zama hizi, tunawaona Jeff Bezos, Mark Zuckerberg na wengine wakijijengea ukiritimba kwenye biashara zao, kiasi cha kutawala soko zima.

Ukiritimba una hasara zake kiuchumi, kwa sababu anayetawala soko anakuwa na nguvu ya kuamua atakavyo, anaondoa ile dhana ya soko huria.

Lakini ukiritimba huo una manufaa makubwa kwa anayetawala, maana hasumbuki na ushindani, anakuwa amelitawala soko na hivyo ananufaika kwa kiasi kikubwa bila kuhofia kuangushwa na wengine.

Kila mmoja wetu anaweza kujijengea ukiritimba kwenye maisha yake, ukamwondoa kwenye ushindani na kumwezesha kutawala kwenye kile anachofanya.

Hilo linaanza na mtu kujitambua mwenyewe, kujua vipaji ulivyonavyo, uwezo wako mkubwa, uimara ulionao na hata madhaifu yako.

Ukishajitambua hivyo, unachagua kufanya kile ambacho kinatumia vizuri rasilimali ulizonazo, ambazo ni wewe pekee unazo dunia nzima.

Badala ya kufanya kazi au biashara kama wengine wanavyofanya, unachagua kufanya kwa upekee, kwa kuweka uhalisia wako kwenye kile unachofanya. Kwa kuwa hakuna mtu anayefanana na wewe dunia nzima, unapokifanya chochote kama wewe, kuna matokeo utakayozalisha ambayo watu hawawezi kuyapata sehemu nyingine yoyote.

Hivyo wanapotaka matokeo hayo, lazima waje kwako. Hata kama wengine wataiga unachofanya, hawataweza kuzalisha matokeo unayozalisha na hivyo bado utabaki kutegemewa katika kuzalisha matokeo hayo.

Unapojitambua, unajua kabisa kuna maeneo ambayo hakuna anayeweza kukushinda hata afanye nini, kwa sababu hakuna aliye kama

wewe, mwenye uwezo, vipaji na uimara ulionao, ambaye amepitia uzoefu kama wako na mwenye ndoto kama ulizonazo.

Unapoweka vitu hivyo pamoja, unakuwa ni moto usioweza kuzimika, unakuwa na nguvu ya kufanya makubwa na kutawala lile eneo ulilochagua.

Kwenye maisha yako, jua ni kitu gani unachoweza kufanya wewe, ambacho hakuna mtu mwingine duniani anayeweza kukifanya, kisha kifanye hicho kwa upekee wa hali ya juu, utakuwa umejijengea ukiritimba wako, utaachana na kushindana na utakuwa na utawala mkubwa kwenye kitu hicho.

## FUNGUA FIKRA ZAKO KWENYE UTELE.

Katika kujitambua, kuchagua eneo la kutawala na kutengeneza ukiritimba wako, kuna fikra unapazwa kuzifuta kabisa kwenye maisha yako, fikra za uhaba.

Unapaswa kufungua fikra zako kwenye utele kwa kila eneo la maisha yako. wakati wengine

wanaona uhaba kwenye kila hali, wewe angalia upande wenye utele. Wakati wengine wanahangaika na mambo wanayoona yana uhaba, wewe usijiunge nao, badala yake hangaika na mambo yenye utele na endelea kutawala maeneo hayo.

Kwa kufungua fikra zako kwenye utele, kuna manufaa makubwa mno ambayo utayapata na yatakusaidia kufanikiwa kwa kiasi kikubwa.

1. Utaacha kushindana na wengine kwa kuwa huamini kuna uhaba, utajua utele wako uliko, ambapo kunaendana na upekee ulionao na utatawala hapo, kitu kitakachokupa mafanikio makubwa.

2. Utaacha kukimbizana na kila fursa mpya ambazo watu wanakuja nazo kwako na kukuambia usipochukua hatua haraka utakosa, kwa kuwa unajua fursa zinazokufaa wewe ni zipi na unajua hakuna uhaba, hutaweza kutapeliwa na fursa mpya zinazokuja kitapeli kila wakati.

3. Utaacha kuwekeza kwa hisia na kuja kupata hasara, pale watu wanapokimbizana na aina fulani ya uwekezaji kwa sababu tu unapanda bei na hawataki kupitwa, wewe utakuwa huangalii kwenye uhaba huo, badala yake unaangalia kwenye utele wako, kitu kinachokuzuia usipoteze pale uwekezaji huo unapokuja kuanguka.

4. Utaacha kuhangaika kununua vitu usivyohitaji kwa sababu tu umeambiwa vina uhaba, kwa kuwa unajua dunia haina uhaba. Unajua chochote unachohitaji utaweza kukipata, kama siyo hicho basi mbadala wake na hivyo watu hawawezi kukusukuma uchukue hatua zisizo na manufaa kwako.

5. Kikubwa zaidi utaishi kwa utulivu na kuweka umakini na nguvu zako kufanya yale yenye manufaa kwako kwa kuwa umechagua eneo sahihi kwako, kuacha kuwaonea wivu wengine kwenye yale waliyochagua maana hayaendani na wewe. Ni utulivu huo ambao kwa muda mrefu utakupa mafanikio makubwa na ambayo hayatatetereshwi kwa namna yoyote ile. Wapo

ambao wanafanikiwa haraka, lakini mafanikio hayo hayadumu kwa kuwa hayakujengwa kwenye msingi sahihi. Wewe utaepuka hilo.

## HITIMISHO.

Asili haijawahi kuwa na uhaba, ila uelewa wetu mdogo ndiyo umekuwa unafanya tuone zaidi uhaba kuliko utele.

Tunapaswa kujitambua sisi binafsi, kujijua kwa undani na kuchagua eneo tutakalotawala na kutengeneza ukiritimba wetu, kisha kuhakikisha wale wenye uhitaji wa tunachotoa wanajua kuhusu uwepo wetu na kuja kwetu ili kukipata, kwa kuwa hawawezi kukipata popote pale.

Tunapaswa kuacha kabisa kufikiri kwa uhaba na kuachana na kila aina ya ushindani, kwa sababu hauna manufaa yoyote kwetu.

Tunapaswa kuwa tayari kuona wengine wakinufaika kuliko sisi badala ya kukimbilia kunufaika kama wao na baadaye kuanguka kwenye hasara kubwa.

Kufikiri kwa utele kunakupa utulivu mkubwa na nafasi ya kujenga mafanikio makubwa na yanayodumu. Mara zote tunapaswa kufikiri kwa utele na siyo uhaba. Hakuna anayeweza kuwa sisi, hivyo tunapaswa kuwa sisi ambao ni bora zaidi kila siku.

# MAONI, SHUHUDA NA MASWALI.

Karibu kwa maoni, shuhuda na maswali kuhusu barua hii.

Kama kuna mahali hujaelewa na ungependa ufafanuzi zaidi basi karibu uulize swali.

Kama kuna eneo unaweza kuongeza maoni zaidi karibu pia.

Na kama una ushuhuda wa namna umewahi kufanyia kazi yale uliyojifunza kwenye barua hii, karibu utushirikishe matokeo ambayo uliyapata.

Maoni, maswali na shuhuda viwekwe moja kwa moja kwenye kundi la KISIMA CHA MAARIFA wasap.

Nikutakie kila la kheri katika kufanyia kazi haya uliyojifunza kwenye barua hii.

Rafiki yako anayekupenda sana,

Kocha Dr. Makirita Amani,

www.amkamtanzania.com/kocha

0755 953 887 / kochamakirita@gmail.com

**MUHIMU;** KAMA HUJAPATA BARUA ZA NYUMA, FUNGUA; www.kisimachamaarifa.co.tz/barua2021